



Bahati Binti Mfalme



Mtunzi: Deogratias Simba
Mchoraji: Michael Sagikwa






Bahati aliishi katika nchi ya Sususu.
Alikuwa binti wa mfalme.
Wazazi wake walikuwa watawala wa Sususu.



Mvua haikunyeshwa kwa muda. Nchi ya Sususu
ilikabiliwa na ukame kwa muda mrefu.
Watu hawakuwa na chakula wala maji.
Mimea ilikauka. Wanyama walitaabika bila maji.



Taabu za wanasususu
zilifika kwa mfalme.
Mfalme na washauri
waliwaza wafanye nini.
Waliitisha kikao kujadili
hali ile.

Bahati alipenda kukaa karibu na baba yake mfalme wa Sususu. Alihudhuria vikao alivyofanya mfalme na washauri wake.







Mfalme alipojadili tatizo la ukame na washauri wake, Bahati naye aliwaza afanye nini kutatua matatizo ya nchi ya Sususu.



Bahati alipata wazo.
Alitaka kumwambia baba
yake, lakini hakumpa nafasi
kwa sababu Bahati alikuwa
mdogo sana.





Bahati alikwenda kwa mama yake, ambaye alikuwa malkia wa Sususu. Malkia alimsikiliza na kuahidi kumsaidia.



Malkia alikwenda kwa mfalme
na washauri wake. Aliwasihi
wasikilize wazo la Bahati.




Mfalme wa Sususu alimpa Bahati nafasi ya kuongea mbele ya washauri. Bahati alisimama mbele ya baraza lile na kueleza wazo lake.




Aliwaeleza watu wa Sususu wazuie maji ya mvua.
Wasiyaache yote yaelekee mtoni. Kisha wachimbe
bwawa la kuyahifadhi.





Pia wazuie maji ya mto na
kuyaelekeza bwawani.
Maji ya bwawani yatawasaidia
hasa kipindi cha ukame.






Mfalme na washauri walifurahishwa na wazo la Bahati. Walipanga kuwaeleza wananchi wa Sususu ili walitekeleze.






Bahati aliwaongoza vijana wa Sususu.
Walichimba bwawa kubwa. Wengine walichimba
mifereji kuelekea bwawani.



Mvua ziliponyesha, mifereji ilipeleka maji bwawani. Mto nao ulitiririsha maji bwawani. Bwawa lilikuwa na maji ya kutosha.



Maji yalifika Sususu.
Watu walipata maji. Mimea
ilinyeshewa. Wanyama walipata
majani na maji. Bahati, Mfalme,
malkia na watu wote wa Sususu
walifurahi sana.